**HOTUBA YA J. S. WARIOBA**

**SIKU YA KUMBUKIZI YA HAKI ZA BINADAMU ILIYOANDALIWA NA LEGAL AND HUMAN RIGHTS CENTRE DAR ES SALAAM,**

**<u>10 DESEMBA 2020</u>**

Nianze kwa kutoa shukrani kwa kukaribishwa kwenye tukio hili muhimu la kumbukizi ya siku ya haki za binadamu. Hii ni siku muhimu kwa dunia nzima.

Baada ya kukubali mwaliko kupitia mkurungenzi Anna Henga nilifikiria kuzungumzia changamoto anazopata mtu ambaye amekuwa mtetezi wa haki za binadamu na ambaye amehusika kwa kiwango fulani katika maandalizi ya mapendekezo au mikataba na sheria kuhusu haki za binadamu, na pia amehusika katika utekelezaji wa mikataba na sheria hizo. Mimi ni mtu wa aina hiyo.

Mwaka 1967 niliteuliwa kuwa mjumbe kwenye jopo lililoandaa mkataba wa Afrika kuhusu wakimbizi. Tulifanya kazi hiyo na mkataba ukakubalika kwenye kikao cha OAU mwaka 1969. Mwaka 1968 nilihudhuria mkutano wa kwanza wa dunia kuhusu haki za Binadamu, Teheran, Iran na 1993 nilihudhuria mkutano wa pili wa haki za binadamu Vienna Austria. Mikutano hiyo ilitoa mapendekezo kuhusu ulinzi wa haki za binadamu.

Mwaka 1979 katika mkutano wa OAU ulifanyika Monorovia, Liberia , niliteuliwa kwenye jopo la kuandaa mkataba wa Afrika kuhusu haki za binadamu (African Charter on Human and People's Rights) na tulipiga kambi Banjul Gambia na kufanya kazi hiyo na nilikuwepo Nairobi, Kenya mwaka 1981 mkataba huu ulipokubaliwa na OAU.

Hapa nyumbani nilishiriki katika maandalizi ya kuingiza sura ya haki za binadamu kwenye katiba mwaka 1983 na mwaka uliofuata katiba ilifanyiwa mabadiliko. Kwa mara ya kwanza haki za binadamu ziliingizwa kwenye katiba ya Tanzania.

Wakati wote huo nilikuwa sehemu ya uongozi wa nchi na nilihusika katika kusimamia utekelezaji wa haki za binadamu. Mwelekeo wangu na matumaini yangu wakati wa maandalizi ya mikataba na sheria yalikumbana na changamoto kiasi cha kusuta nafasi yangu. Lakini hiyo ni hadithi ya baadaye. Leo napenda nizungumzie AMANI.

Kama msemo uendavyo AMANI NI TUNDA LA HAKI, palipo na haki kuna amani. Ni ukweli pia kwamba pasipo na amani haiwezekani kuwa na haki. Katika nchi ambazo kuna vurugu haki za watu huingiliwa. Katika dunia ya sasa vyanzo vya vurugu ni vingi. Chanzo kimoja wapo kikubwa ni siasa. Katika miaka kumi iliyopita dunia imeshuhudia vurugu za kisiasa ambazo zimeingilia sana haki za binadamu.

Kati ya mwaka 2010 na 2012 yaliotokea matukio mengi ya kisiasa katika nchi za Arabuni ambayo yaliitwa Arab Spring. Nchi nyingi zilihusika Tunisia, Libya, Misri, Yemen, Syria, na nyingine. Kulikuwa na maandamano mengi na watu wengi walipoteza maisha. Inakisiwa watu zaidi ya laki moja kutoka nchi hizi walipoteza maisha na wengi zaidi walipata madhara ya aina mbalimbali.

Vurugu za aina hiyo zimeendelea kutokea na zinatokea hivi sasa tunavyozungumza katika nchi kama Belarus, Armenia, Azerbaijan, Thailand, Hong Kong, Ethiopia, Myanmar na kadhalika. Vurugu zinazotokana na uchaguzi nazo zinatokea katika nchi nyingi. Hivi karibuni tumeona vurungu zimetokea Malawi, Senegal, Mali, Uganda, Marekani na sehemu nyingine. Watu wamepoteza maisha na kupata madhara mengine. Hivi sasa Uganda iko kwenye kipindi cha kampeni na tayari watu karibu hamsini wamepoteza maisha.

Hapa nyumbani tunazo changamoto, hasa wakati wa uchaguzi. Zanzibar imekuwa na changamoto hizi tangu wakati wa ukoloni. Uchaguzi wa Zanzibar kabla ya uhuru ulikuwa na matatizo. Baada ya kurudisha mfumo wa vyama vingi matatizo yalizuka tena. Uchaguzi wa 1995 uliwagawa wananchi wa Zanzibar mpaka wakafikia hatua ya ndugu kususiana. Baada ya uchaguzi wa 2000, zilitokea vurugu, watu walipoteza maisha na wengine wakaikimbia nchi. Uchaguzi wa 2015 ulifutwa na

vurugu za 2020 zilikuwa chanzo cha watu kupoteza maisha Pemba na Unguja.

Kwa upande wa Tanzania Bara hakukuwa na matatizo makubwa kwa muda mrefu. Kila baada ya uchaguzi tathimini ilifanywa ili kubaini udhaifu uliojitokeza na marekebisho yalifanywa. Kwa miaka mingi hazikutokea vurungu za kuleta madhara makubwa. Lakini uchaguzi wa mwaka huu umekuwa chanzo cha vurugu katika sehemu mbalimbali. Watu wamepoteza maisha Tarime, Tunduma na Ukerewe na wengine wameumizwa na mali kuharibiwa.

Ni jambo la kawaida kufanya tathimini kila baada ya uchaguzi na kubaini kama kuna haja ya kufanya mabadiliko ya sheria, kanuni au taratibu za mchakato wa uchaguzi.

Naamini wanaohusika watafanya tathimini ili kugundua udhaifu uliojitokeza na baada ya hapo mabadiliko yatafanywa kwenye kanuni, taratibu na sheria za uchaguzi. Jambo hili ni muhimu kwa sababu kama hatua zisipochukuliwa uchaguzi utakuwa chanzo cha vurugu za kuhatarisha amani ya nchi.

Katiba ya Tanzania katika ibara ya 5, inaeleza haki ya kila raia mwenye umri wa miaka kumi na nane kupiga kura. Ibara ya 21 inaeleza haki ya raia ya kushiriki katika shughuli za utawala wa nchi ama moja kwa moja au kwa kupitia wawakilishi. Mchakato wa uchaguzi ni njia ya

kutekeleza haki za raia. Uchaguzi wa mwaka huu umekuwa na udhaifu katika utekelezaji katika maeneo fulani fulani.

Kwa haraka haraka naona kuna maeneo manne ya kuangalia. Eneo la kwanza linahusu vyama vya siasa. Utaratibu wa kuteua wagombea unaanza ndani ya vyama vya siasa. Kila chama cha siasa kina utaratibu wake lakini kila chama kinatakiwa kuzingatia umuhimu wa kuteua wagombea wanaokubalika na wananchi. Kwa hali ya sasa matakwa ya wananchi hayazingatiwi sana. Vyama vinajali zaidi masilahi yao na pia kuna matumizi makubwa ya fedha, yaani rushwa. Matokeo yake ni kwamba watu wengi wanaokubalika na wananchi hawateuliwi.

Kwenye kitongoji, kwa mfano, wananchi wanafahamiana na wanajua nani anaweza kuwa kiongozi wao. Kwa taratibu za sasa watu wasiokubalika huteuliwa. Hali ndivyo ilivyo kuhusu uongozi mzima wa vijiji na mitaa, kata na hata jimbo la uchaguzi. Matokeo yake wananchi wanapoteza imani na baadhi yao wanasusa kupiga kura na wengine wanakuwa wepesi kufanya fujo wakishawishiwa. Na viongozi wanaochaguliwa wanakosa ushirikiano wa wananchi katika shughuli za maendeleo. Ni vema vyama vya siasa vikafanya tathimini ili kuleta mabadiliko ambayo yatalenga kupata wagombea wanaokubalika na wananchi na pia kuzuia rushwa katika mchakato wa uchaguzi.

Eneo la pili linahusu Tume ya Uchaguzi. Mwaka huu 2020 Tume ilifanya maandalizi mazuri sana. Ilitoa elimu ya kutosha kuhusu uandikishaji wa wapiga kura na daftari la wapiga kura lilikamilishwa bila malalamiko. Vifaa na vituo vya kupiga kura viliandaliwa vizuri. Idadi ya vituo iliongezwa kupunguza msongamano. Watumishi wa Tume waliwasaidia wapiga kura na upigaji kura ulikwenda vizuri. Tatizo lililotokea wakati wa uteuzi wa wagombea. Ili mtu ateuliwe kuwa mgombea ni lazima awe na sifa za msingi. Sifa hizo ambazo ziko kwenye kifungu cha 67 cha Katiba kuhusu wabunge ni pamoja na kuwa raia mwenye umri wa miaka ishirini na moja au zaidi, anajua kusoma na kuandika Kiswahili au Kiingereza, amependekezwa na chama cha siasa, hana ugonjwa wa akili na hajapatikana na hatia ya makosa ya aina fulani kama vile kukwepa kodi au kukosa uaminifu au amefungwa jela kwa kipindi kinachozidi miezi sita. Wagombea pia wanatakiwa kupata wadhamini kama ishara ya kukubalika na jamii. Mwisho wanatakiwa kuapa. Haya ndiyo masharti yaliyo ndani ya Katiba na sheria.

Huko nyuma si wagombea wengi walienguliwa wakati wa uteuzi. Ghafla mwaka 2019 kwenye uchaguzi wa Serikali za mitaa wagombea wengi walienguliwa. Mwaka huu Tume iliengua wagombea wengi sana. Taarifa zinaonyesha kwamba wagombea hawakuenguliwa kwa sababu hawakuwa na sifa za msingi. Wengi walienguliwa kwa makosa madogo madogo ya kujaza fomu. Tume ya uchaguzi ina jukumu la kutafakari suala

hili na kufanya mabadiliko. La sivyo itaonekana Tume imeweka pembeni masharti ya Katiba na kujitungia ya kwake. Imani ya wananchi itapungua na wanaweza kuingia kwenye vitendo vya kuleta vurugu.

Eneo la tatu nalo linahusu Tume ya Uchaguzi. Mgombea ana haki ya kuwa na wakala kwenye kila kituo cha kupigia kura. Wakala anateuliwa na mgombea au chama chake. Kazi ya Tume ni kuthibitisha kwamba wakala anakubalika na mgombea na chama chake. Katika uchaguzi uliopita Tume iliengua mawakala wengi kwa kufuata taratibu ilizojiwekea. Mwisho ikaonekana kama mawakala ni wa Tume Jambo hili linaweza kuwa ni chanzo cha baadhi ya wananchi kutoridhika na kujiingiza kwenye vitendo vya kuhatarisha amani.

Eneo la nne ni utaratibu wa kusikiliza malalamiko na kutoa maamuzi wakati wa kampeni. Tume ya Uchaguzi imeunda chombo cha kupokea malalamiko kuhusu makosa yanayotendwa na wagombea wakati wa kampeni. Chombo hicho ni kama mahakama. Wajumbe wake ni pamoja na wawakilishi wa Vyama vya Siasa. Mahakama hii inatoa adhabu, ikiwa ni pamoja na kumfungia mgombea asiendeshe kampeni kwa muda fulani. Ni vigumu kuamini kwamba chombo ambacho wajumbe wake ni washindani kinaweza kutenda haki. Ni vema Tume ikaweka utaratibu mwingine ambao utaonekana kutenda haki bila mashaka.

Amani tuliyonayo ilijegwa kwa msingi wa Imani ya utu. Waasisi waliamini binadamu wote ni sawa. Kwa msingi huo walianza kuondoa ubaguzi wa kila aina. Ubaguzi wa rangi dini na makabila uliondolewa.kiswahili kilifanywa lugha ya taifa. Jitihada kubwa zilifanywa kujenga umoja na umoja huo ndio ulileta amani.

Tangu mwanzo Katiba ya nchi ilizingatia misingi kwamba madaraka ya nchi yanatokana na wananchi. Wananchi ndio wenye mamlaka ya kuchagua wawakilishi kwenye vyombo vya kutunga sheria. Kati ya sababu zilizotolewa za kuanzisha mfumo wa demokrasia ya chama kimoja ni kuhakikisha wananchi wanapata nafasi ya kupiga kura. (sababu kubwa ilikuwa kujenga umoja waasisi waliamini kwamba mfumo wa vyama vingi unaleta mgawanyiko).

Katika uchaguzi uliofanya kabla ya uhuru wananchi wengi hawakupata nafasi ya kupiga kura kwa sababu wagombea wengi walipita bila kupigwa. Chini ya mfumo wa demokrasia ya chama kimoja kulikuwa na ushindani katika kila jimbo. Wakati huasilimia kubwa ya waliojiandikisha kupiga kura walijitokeza na kupiga kura kwa amani kabisa.

Amani na umoja wa Watanzania ilijengwa kwa ushawishi wa viongozi hasa viongozi wa kisiasa. Baada ya hapo matendo ya viongozi yaliendana na kudumisha amani na umoja. Kulikuwepo na viongozi wa

siasa waliojaribu kutumia ubaguzi wa rangi, dini na ukabila lakini vitendo vyao vilikemewa. Kwa ujumla viongozi walifanya kazi kwa pamoja bila ubaguzi.

Baada ya kurudisha mfumo wa vyama vingi vya siasa, viongozi wamekuwa chanzo kimojawapo cha mgawanyiko

Ndani ya jamii. Vyama vya siasa vimekuwa kama makabila yenye uhasama. Ubaguzi wa dini, ukabila na hata ukanda unajitokeza. Huko nyuma Watanzania walikuwa wamezoea amani na walikuwa hawaizungumzii. Hivi sasa suala la kulinda amani linahubiriwa na wengi na kila wakati. Ni wazi kuna hatari ya amani kutoweka.

Mara nyingi wito unatolewa kwa wananchi kulinda na kudumisha amani na umoja. Lakini tatizo haliko kwa wananchi. Wananchi katika maisha yao ya kawaida vijijini na mijini hawabaguani. Wanaendesha shughuli zao za maendeleo kwa pamoja na kwa amani. Mtu akienda kwenye sehemu za mikusanyiko hatakuta ubaguzi. Kwenye masoko hapa Dar es Salaam, kama vile Kariakoo, Tandale, Ilala, Temeke, Magomeni na kadhalika wananchi wanafanya shughuli zao bila kuulizana dini, kabila,

kanda na bila kujali rangi. Ikiingia siasa ndipo migawanyiko inaanza. Siasa iliwagawa wafanyabiashara wa soko la Darajani, Zanzibar kati ya wakeleketwa na wafurukutwa hadi wakawa wanasusiana.

Viongozi wa dini wamejitahidi sana kuhubiri amani na umoja. Viongozi wa dini mbalimbali wameunda hata kamati za kulinda amani. Ni jadi ya viongozi wa dini kuhubiri amani. Kwenye makanisa na misikiti amani huhubiriwa wakati wote. Kwa Wakristo salaam za mwisho za padre, mchungaji au askofu ni "nendeni na amani". Kama nilivyoeleza umoja na amani ya nchi hii vilijengwa na viongozi wa kisiasa na baada ya hapo wakalinda amani hiyo. Litakuwa jambo jema kama viongozi wa kisiasa wakaiga kinachofanywa na viongozi wa kidini. Ni wazi kwamba umoja wetu na amani yetu vimo katika hatari ya kuvunjika. Itakuwa jambo jema kama wakikaa pamoja bila kujali vyama na kutafakari jinsi ya kulinda umoja na amani yetu.

Siyo vizuri kuliachia jambo hili kubwa kwa viongozi wa dini na viongozi wa vyombo vya dola kama polisi. Polisi hawaleti amani, polisi

wanalinda amani. Kazi ya polisi ni kusimamia sheria, kudhibiti uhalifu na kulinda wananchi na mali zao. Polisi ni chombo cha kutumia nguvu ya sheria na siyo chombo cha ushawishi. Kazi hii imefanywa vizuri na polisi kwa kiwango kikubwa. Ni vema polisi wakaachiwa kufanya kazi yao na wasiingizwe kwenye malumbano ya kisiasa.

Nchi yetu ina tabia ya kukabili matatizo kwa uwazi bila kusita. Hivi sasa kuna viashiria vya uvunjifu wa amani. Zipo sheria nyingi za kulinda haki za binadamu. Zipo pia taasisi nyingi kwa madhumuni hayo hayo. Matatizo mengi yanataokana na utekelezaji. Tunaweza kushughulikia matatizo haya na kufanikiwa kukiwa na amani.

Ushirikiano mzuri unahitajika kati ya viongozi wa kisiasa. Ushirikiano pia unahitajika kati ya vyama vya vya siasa. Hali ya sasa inatawaliwa na uhasama, kejeli, kebehi na matusi. Hali nzuri inayohitajika ni ushindani wa hoja.

Ushirikiano wa taasisi nao unahitaji mabadiliko. Uhusiano wa Tume ya uchanguzi na vyama vya siasa ni wa mvutano. Hali ni hiyo kati ya Ofisi

ya Msajili na Vyama Vyama Siasa. Lakini majukumu ya taasisi hizi ni kutumikia wananchi kwa pamoja. Mvutano wa taasisi hizi unagawa wananchi. Kwa mfano wanachama na washabiki wa Vyama wamegawanyika kwa kufuata matamko na matendo ya viongozi wao. Kama kiongozi watashirikiana, wananchi nao watashirikiana. Kwa mfano wananchi wa Zanzibar waligawanyika sana lakini baada ya Rais Karume na Maalim Seif kuonyesha ushirikiano wananchi nao wakaanza kuwa na uhusiano mzuri. Litakuwa jambo jema kama viongozi wa dini wanavyofanya ili kupata suluhu ya kuvunjika kwa amani na kuweka msingi mzuri wa kulinda haki za binadamu.